**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA MJI WA BABATI

(*Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji*)

# TAARIFA KWA UMMA

## MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO NJE YA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KIASI CHA SHILINGI 584,000,000.00

Katika mwaka wa fedha, 2024/2025, Halmashauri ya Mji Babati kupitia Bajeti ya miradi ya maendeleo kwa chanzo cha fedha za Serikali Kuu, fedha za ndani iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 450,000,000.00**, Serikali ilishatoa fedha hizi kwa asilimia 100.

Pamoja na mapokezi haya ya fedha za maendeleo zilizokuwa katika bajeti ya mwaka 2024/2025, Serikali imetoa fedha ambazo hazikuwa kwenye bajeti kiasi cha **shilingi 584,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi mpya na ukamilishaji wa maboma katika sekta za Elimu Msingi na Sekondari. Fedha hizi zimepokelewa kati ya mwezi Aprili na Mei, 2025.

Kutokana na kwamba fedha hizi hazikuwa na vifungu vya matumizi, Halmashauri imeshafanya taratibu zote na tayari vifungu vya matumizi ya fedha hizi vimepatikana tayari kwa matumizi.

Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hizi ni kama ifuatavyo:

| Na. | Jina la Mradi | Mahali ulipo (Kata) | Kiasi pokelewa |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Elimu Msingi** | | |
| 1.1 | Ujenzi wa Kituo cha walimu (Teachers' Resource Centre) shule ya Msingi Harambee | Bagara | 54,000,000.00 |
| 1.2 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya Msingi Sora | Mutuka | 50,000,000.00 |
| 1.3 | Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa shule ya msingi Daghailoy | Sigino | 25,000,000.00 |
| | **Jumla** | | **129,000,000.00** |
| **2.0** | **Elimu Sekondari** | | |
| 2.1 | Ujenzi wa mabweni 2 na vyumba 2 vya madarasa sekondari ya Nakwa | Bagara | 310,000,000.00 |
| 2.2 | Ukamilishaji wa bweni Sekondari ya Babati day | Bagara | 40,000,000.00 |
| 2.3 | Ukamilishaji wa bweni Sekondari ya Kwaang'w | Maisaka | 20,000,000.00 |
| 2.4 | Ukamilishaji wa chumba cha maabara sekondari ya Mutuka | Mutuka | 30,000,000.00 |
| 2.4 | Ukamilishaji wa chumba cha maabara sekondari ya Nangara | Nangara | 30,000,000.00 |
| 2.5 | Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa sekondari ya Komoto | Bagara | 25,000,000.00 |
| | **Jumla Sekondari** | | **455,000,000.00** |
| | **Jumla Kuu** | | **584,000,000.00** |